**JIMBO KATOLIKI MOSHI.**

**SHULE YA SEKONDARI OLALENI**

**S.L.P 176, HIMO - MOSHI.**

*SIMU Na. 0272758836, - OFFICE*
*0657 987292 / 0756 955080, - MKUU WA SHULE*
*0759 609104 / 0783 572045, - MAKAMU MKUU WA SHULE*
*0758 587288, - KARANI/ SECRETARY*
*0762 803044 / 0753 638513 – TAALUMA*
*0752 253260 / 0718 215713 – MHASIBU*
*E –mail: olalenisecon@gmail.com*
*Website : www.olalenisecondary . sc. Tz*

PICHA

(PASSPORT)

**Kumb. Na. OSS/HG/VOL-02/225.**

Jina kamili la Mwanafunzi ..........................................................................................

**YAH: MAAGIZO YA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA (I) MWAKA 2026.**

1. Mmiliki na Meneja wa shule Baba Askofu Jimbo Katoliki Moshi, Bodi ya shule pamoja na Jumuiya nzima ya Olaleni Sekondari wanayofuraha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Olaleni kidato cha kwanza mwaka **2026**. Tarehe ya kufungua shule ni **05/01/2026** kwa bweni na kutwa ni **06/01/2026**. Wanafunzi watapokelewa siku hiyo kuanzia saa **4:00** asubuhi hadi saa **10:00** jioni. Tafadhali zingatia muda na tarehe iliyopangwa.
   Shule ipo Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Moshi Vijijini, Kata ya Kilema, kilometa **9** kutoka barabara kuu inayoelekea Himo.

2. **ADA:-** Wanafunzi wa **Bweni**(kulala) kwa mwaka **1,800,000/= (**MILIONI MOJA NA LAKI NANE)
   Wanafunzi wa **Kutwa** kwa mwaka **1,000,000/= (**MILIONI MOJA**)**

| NA. | MAELEZO | MUHULA I | MUHULA II | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| i | Wanafunzi wa Bweni (**Kulala**) | 900,000/= | 900,000/= | **1,800,000/=** |
| ii | Wanafunzi wa Kutwa (**Day Scholar**) | 500,000/= | 500,000/= | **1,000,000/=** |

**NB:** Ada iliyotajwa hapo juu inajumuisha michango yote inayotozwa shuleni. **Fedha za Ada ziwekwe kwenye akaunti ya shule OLALENI SEC. SCHOOL Na. 01J1039824000 CRDB/au Na. 00510503704801 MKOMBOZI COMMERCIAL BANK. na siku ya kuripoti uje na "Pay in Slip" ya malipo toka benki uliyolipia. Usilete pesa taslimu hapa shuleni hazitapokelewa.**
**(Kumbuka kuandika Jina na kidato cha Mwanafunzi pindi ufanyapo malipo yoyote katika Benki zilizotajwa).**

3. **MALIPO YA BIMA YA AFYA** -Tshs. **52,000/=**
   Hii ni kwa wanafunzi wote wasio na Bima ya afya za wazazi/walezi.

4. **SARE (UNIFORM).**

A. **WASICHANA**.

| | | |
|---|---|---|
| (i) Sketi 2 | Tshs. | **44,000/=** |
| (ii) Shati 2 | Tshs. | **20,000/=** |
| (iii) Gauni 2 (za kushindia) | Tshs. | **36,000/=** |
| (iv) Truck Suit 2 (za jioni) | Tshs. | **50,000/=** |
| (v) T-shirt 2 ("polo" za darasani" | Tshs. | **30,000/=** |
| (vi) Shuka jozi 1 na foronya zake | Tshs. | **24,000/=** |
| (vii) Sweta 1 (ya darasani) | Tshs. | **20,000/=** |
| **JUMLA** | | **224,000/=** |

B. **WAVULANA.**

| | | |
|---|---|---|
| (i) Suruali 2 (za darasani) | Tshs. | **44,000/=** |
| (ii) Suruali 2 (za kushindia) | Tshs. | **44,000/=** |
| (iii) Shati 2 | Tshs. | **20,000/=** |
| (iv) Truck Suit 2 (za jioni) | Tshs. | **50,000/=** |
| (v) T-shirt 2 ("polo" collar za darasani) | Tshs. | **30,000/=** |
| (vi) T -shirt 2 ("round" collar za kushindia) | Tshs. | **20,000/=** |
| (vii) Shuka jozi 1 na foronya zake | Tshs. | **24,000/=** |
| (viii) Sweata 1 (ya darasani) | Tshs. | **20,000/=** |
| **JUMLA** | | **252,000/=** |

Bei ya sare hizi inajumuisha kuweka nembo na alama kwa kila sare ya mwanafunzi ili kudhibiti wizi.

**Fedha za Bima ya Afya, Sare (uniforms), na matumizi binafsi zilipwe kwenye akaunti ya "Pocket money" Na. 0150039824001 CRDB – Jina la akaunti OLALENI SEC. SCHOOL.**

**(Kumbuka kuandika Jina na kidato cha Mwanafunzi pindi ufanyapo malipo yoyote katika Benki iliyotajwa).**

Baada ya mwanafunzi kuripoti shuleni atatakiwa kufungua "**Mtoto Account**" katika benki ya CRDB kwa ajili ya kuhifadhi fedha zake za matumizi.

5. **A. KWA WALE WA BWENI WAJE NA VIFAA VIFUATAVYO:-**

i **Godoro** Jipya lenye foronya na liwe na Jina kamili la mwanafunzi lenye urefu **futi 6**, upana **futi $2^1/_2$** na unene **inch "4" – "6".**

ii Blanketi, Chandarua, Mto, taulo, kanga/Kitenge doti moja (I) kwa wasichana.

iii Nguo za michezo wasichana T-shirt ziwe za blue (yaweza kuwa aina ya "**Jersey**") na sketi nyeusi ya mshono wa "**Solo**". Wavulana wawe na T-shirt za blue na bukta za blue (**Jersey**).

iv **Raba** za michezo kwa wasichana na wavulana.

v Counter Books **12** (**Quire 2 au 3**).

vi English Dictionary (**English to English – Oxford/ Macmillan/ Longman**).

vii Biblia na vitabu vingine vya dini kulingana na dhehebu lake **Kwa Wakatoliki – RC waje na Biblia yenye vitabu vya Deuterokanoni** na kitabu cha dini Kidato cha kwanza (Elimu ya Dini Katoliki na Maadili shule za sekondari).

viii Sanduku dogo la bati (**Tranka**) pamoja na kofuli lake. **NB**. "**Mabegi"** au "**Suitcase**" hayaruhusiwi.

ix Mathematical Set.

x Mkoba wa Madaftari ( **School Bag** or **Backpack**).

xi Sahani, kikombe, bakuli na kijiko. **Visiwe vyombo vya "Plastics".**

xii Ndoo na iwe na jina lake pamoja na Ndala za kuogea.

xiii Mpira mpya (**Markin tosh**) kwa wale wenye matatizo ya kukojoa kitandani na shuka za ziada kwa ajili ya usafi binafsi.

xiv Viatu jozi mbili (**2**) vyeusi na viwe na kamba za kufungia.

xv Soksi jozi mbili (**2**) ndefu na ziwe nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.

xvi "**Sandals**" au "**Simple shoes**" za kuvaa baada ya saa za masomo kwa wasichana na wavulana.

xvii Shati **Jeupe** la **mikono mirefu** (kwa ajili ya kuvaliwa siku maalumu).

xviii Nguo za kulala na mavazi ya ndani ikiwemo "**underskirts**" kwa wasichana.

xix Sabuni za kuogea na za kufulia nguo. (**ambazo hazina manukato / marashi**).

xx Mafuta ya kupaka ngozi yawe ni mgando jamii ya "**Vaseline**" "**Body care**" "**Babycare**" na yasiwe na manukato/marashi. **("creams" na "lotion" haziruhusiwi**).

xxi Fedha za matumizi yake binafsi (**Pocket Money**) zisiwe kidogo sana au nyingi sana, Fedha za matumizi hutunzwa na shule. Endapo mwanao hatafuata utaratibu huu, fedha zake zikapotea shule haitahusika.

## B. <u>MAELEZO MUHIMU;-</u>

a) Vifaa vya muziki, Kamera, Simu, Redio, Albamu za picha, Midoli, Vyakula, Vinjwaji n.k haviruhusiwi na akikamatwa navyo atakuwa amejiondoa shuleni.

b) Mavazi ya gharama (**Kifahari**) hayaruhusiwi hapa shuleni.

c) Shule haigharamii nauli ya mwanafunzi wakati wa likizo fupi au ndefu, ila huandaa usafiri kwa wanafunzi wote. Ni sheria ya shule kwa mwanafunzi kuondoka shuleni chini ya usimamizi wa mwalimu husika.

d) Mwanafunzi akifukuzwa au kurudishwa nyumbani hugharamia usafiri wake mwenyewe .

e) Endapo mwanao ana tatizo la kiafya aje na uthibitisho wa daktari.

f) Shule haina huduma ya mlo maalumu (**Special diet**).

g) shule inatoa huduma ya kwanza ila endapo mwanafunzi atalazwa hospitalini au kupelekwa hospitali ya rufaa basi mzazi/mlezi atagharamia matibabu na gharama nyingine zitakazojitokeza.

h) Hakikisha unasoma viambatanisho vya **Tamko rasmi la mzazi na mwanafunzi** na **fomu ya Daktari** (Medical Examination) zijazwe kikamilifu.

i) Ada ikishalipwa hairudishwi. Ada ya muhula lazima ilipwe yote ili kuepuka mwanao kurudishwa nyumbani mara kwa mara.

Mwisho ninakukaribisha sana shuleni ufike na fomu hii. Hakikisha unasoma fomu hii na mwanao na kuielewa na ukienda kinyume na maagizo hayo mwanao hatapokelewa shuleni na nafasi yake atapewa mtu mwingine. Mwanao pia awe tayari kufuata kanuni na sheria za shule muda wote awapo shuleni la sivyo anaweza akapoteza nafasi yake ya masomo.

# SHERIA ZA SHULE.

Shule ya Sekondari Olaleni ni shule ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana "**Day"** na "**Boarding".** Iko chini ya Jimbo Katoliki Moshi ambapo Meneja na Mwenye shule ni Mhashamu Baba Askofu wa Jimbo Katoliki Moshi.

Shule hii kama zilivyo shule zote za Sekondari nchini, ina msimamo mmoja katika masuala yote ya taaluma, nidhamu na kanuni za uendeshaji. Hivyo basi sheria na kanuni za shule ni lazima zizingatiwe ili kuboresha malengo ya elimu itolewayo kwa manufaa ya Taifa. Ukikiuka sheria hizi ni sawa na kujiondoa mwenyewe katika jumuiya ya shule hii.

1. **HESHIMA.**
   - (a) Kila mwanafunzi ni lazima asimame na kutoa salamu kwa heshima kwa wote waliomzidi umri kwa kutumia lugha ya kiingereza awapo shuleni.
   - (b) Mwanafunzi asitumie lugha mbaya, wakati wowote kati yake na mwenzake, kwa walimu wake ama kwa mtu yeyote.
   - (c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kwao kama walimu na walezi wao wengine
   - (d) Kila mwanafunzi ni lazima ashirikiane na wenzake katika kazi zote anazopangiwa na uongozi wa shule
   - (e) Hairuhisiwi kwa mwanafunzi yeyote akiwa shuleni;-
     - (i) Kuvuta sigara ya aina yoyote, bangi wala ugoro
     - (ii) Kufuga nywele ndefu
     - (iii) Kufuga kucha ndefu
     - (iv) Kufuga ndevu
     - (v) Kupaka kucha rangi
     - (vi) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
     - (vii) Kuvaa mavazi ya kiraia
     - (viii) Kugombana au kupigana nje au ndani ya shule wakati wowote
     - (ix) Kunyoa mitindo isiyo rasmi mf. "**Kiduku**" "**Punky**"
     - (x) Kubadilisha nywele kwa kupaka madawa
     - (xi) Kubadilisha rangi ya ngozi kwa kutumia vipodozi
     - (xii) Kusuka nywele
     - (xiii) Kuiba
     - (xiv) Kuchora michoro katika mwili mfano "**tatoo**"
     - (xv) Mahusiano ya Kimapenzi, wote mnapaswa kuishi kama ndugu au kaka na dada kwa hivyo ni kosa kwa mwanafunzi kuonesha kwa namna yoyote ile kwamba wanaishi kama mtu na mpenzi wake au mchumba.
   - (f) Kila mwanafunzi ni lazima kuitikika mara moja na kufuata wito unaotakiwa na mwalimu au mlezi aliyemwita
   - (g) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, bendera za vyama vyote vilivyosajiliwa, Nembo ya Taifa, picha za viongozi wa vyama na serikali, wimbo wa Taifa na Fedha za taifa.
   - (h) Ni lazima kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia, darasani, ofisini, mali binafsi na mali za shule
   - (i) Ni lazima kusimama katika mistari wakati wa kupokea huduma
   - (j) Ni lazima kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote alipo

(k) Nyoosha mkono juu na simama unapoulizwa na kujibu swali

(l) Kaa kimya wakati wote unapokuwa darasani, usitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.

(m) Ni marufuku mwanafunzi kuhudhuria sherehe zozote isipokuwa zilizokubaliwa na shule

(n) Ni hatia kupeleka habari au kuandika barua yenye hila kwenye vyombo vya habari bila kupitia kwa Mkuu wa Shule

(o) Wanafunzi wanapaswa kupita/ kutumia tu njia zilizowekwa ndani ya mazingira ya shule. Hairuhusiwi kukatiza kwenye maeneo maalumu mfano;- Viwanjani, bustani na maeneo yaliyotengwa.

(p) **“Kumcha Mungu ni chanzo cha Maarifa”** Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vya dini, sala wakati wa asubuhi na jioni, pia ibada kwa siku zilizopangwa kwa kadiri ya utaratibu wa shule. Pia mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini au dhehebu awapo shuleni

(q) Ni marufuku kupeleka na kula chakula bwenini au darasani bila kibali maalumu. Vyakula na vinjwaji vitumiwe kwenye bwalo la chakula.

**2. MAHUDHURIO.**

(i) Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie shule kwa muda wote wa masomo. Siku za masomo darasani zisipungue **194**

(ii) Ni lazima kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ipasavyo pia kufavya mazoezi, majaribio, na mitihani yote itakayotolewa. Ni marufuku kupiga kelele, kuandika barua, kuandika ubaoni bila ruhusa wakati wa masomo na maandalio ya jioni.

(iii) Ni lazima kuhudhuria na kufanya kazi zote za mikono

(iv) Ni lazima kuhudhuria mikutano yote ya shule, kama vile Baraza la shule, matangazo, shughuli za usafi, na shughuli yoyote ya dharura kila inapotokea

(v) Kila mwanafunzi ni lazima awe kwenye “**ROLL CALL**” yoyote inayoitishwa

(vi) Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shuleni kwa siku sitini atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.

(vii) Kila mwanafunzi sharti awahi wakati wote anapohitajiwa darasani, mstarini, bwaloni, katika kazi za nje anapoitwa kwa kengele au ishara nyingine. Hii inahusu pia kuwahi kurudi shuleni mwisho wa likizo.

**3. KUWAHI.**

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku. Watakaochelewa watachukuliwa hatua za kinidhamu.

(ii) Ni lazima kuwahi mara usikiapo wito wa dharura.

(iii) Ni lazima kufika shule kwa tarehe na muda uliopangwa.

**4. SARE YA SHULE.**

(i) Ni lazima kila mwanafunzi kuvaa sare ya shule wakati wa;-

(a) Masomo ya darasani
(b) Anapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
(c) Anapokuwa kwenye Baraza la shule au kwenye mhadhara wowote wa shule
(d) Anapohudhuria maandamano yaliyopangwa na Taifa.
(e) Anapokwenda hospitalini
(f) Anaposafiri kuja shuleni au kwenda nyumbani.

**5. MIPAKA YA SHULE.**

(i) Mwanafunzi yeyote akiwa shuleni haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalumu cha Mkuu wa Shule

(ii) Iwapo mwanafunzi ameruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule anatakiwa kurudi mara moja kwa muda aliopangiwa.

(iii) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembea au kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa.

a) Chumba cha walimu (**Staff room**)
b) Ofisi za shule
c) Maabara
d) Jikoni
e) Nyumba za kuishi walimu na wafanyakazi wasio walimu.

(iv) Ni marufuku kwa ;-

a) Wavulana kuingia au kuonekana katika eneo la bweni la wasichana
b) Wasichana kuingia ndani ya bweni la wavulana.

(v) Ni marufuku kutembea au kuingia kwenye sehemu zifuatazo;-

a) Vilabu vya pombe
b) Majumba ya starehe
c) Majumba ya kufikia wageni “**Guest House”**

Makosa yanayoweza kumsimamisha au kumwondoa shuleni au kufukuzwa shule kabisa kwa mwanafunzi;-

- Mimba, uasherati na uzinzi
- Kuchezea au kuharibu bendera ya Taifa au picha za Viongozi
- Kutoroka, kuruka ukuta na kulala nje ya shule
- Wizi
- utoro
- Ulevi wa aina zote
- Kukataa adhabu
- Ugomvi au kupigana
- Kuibia mitihani
- Kuongoza mgomo au kufanya ghasia shuleni
- Kuharibu mali ya Umma kwa makusudi
- Kuweka au kuvuta bangi
- Makosa yote ya jinai yaliyodhibitishwa na mahakama
- Kutoroka vipindi vya darasani
- Kushindwa kufanya mitihani
- Kuwa/kutumia simu ya mkononi ndani ya shule

Pamoja na sheria na taratibu hizi zote, unatakiwa kufuata katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania.

…………………

***VICTORIA J. MATOLI***

***MKUU WA SHULE.***

**CATHOLIC DIOCESE OF MOSHI**
**OLALENI SECONDARY SCHOOL**
**P.O. BOx 176 HIMO – MOSHI.**

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

**To Medical Officer.**

……………………………………………………

…………………………………………………..

…………………………………………………..

Pupils Name ………………………………………………………………………………….. Date …………………………………………..

Form ………………………………………………………………………………………………………………………………………………

**Blood coast (Red & White)**

Stool examination ……………………………………………………………………………………………………………………..

Urinal analysis …………………………………………………………………………………………………………………………..

Syphilis Test ………………………………………………………………………………………………………………………………

Eye Test ……………………………………………………………………………………………………………………………………..

Ears ……………………………………………………………………………………………………………………………………………..

Chest …………………………………………………………………………………………………………………………………………..

Spleen …………………………………………………………………………………………………………………………………………

Abdomen …………………………………………………………………………………………………………………………………….

**(Check cases of pregnancy in girls)**

Additional information e.g. Physical defects or impairments infection, chronic or family disease **etc.**

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………………….

**MEDICAL CERTIFICATE.**

**(To be complete by Medical Officer)**

**Name** ………………………………………………………………….. **Station** ……………………………………………………………..

**Date** **…….**…………………………………………………………… **Signature** ………………………………………………………….

Note to Medical Officer at the time of examination please treat the individual.

**FOR ANY ALIMENT YOU NOTE** ………………………………………………………………………………………………….

**JIMBO KATOLIKI MOSHI.**
**OLALENI SEKONDARI**
**S.L.P 176 HIMO – MOSHI.**

## SEHEMU HII IJAZWE NA IRUDISHWE SHULENI

## TAMKO RASMI LA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI.

(I) **MWANAFUNZI.**

Mimi ________________________________________ Ninayeomba kusajiliwa katika shule ya Sekondari Olaleni naahidi kufuata sheria zote za shule na kushika maadili ya dini na kama nitavunja sheria yoyote nichukuliwe hatua stahili. Ninaahidi kusoma kwa bidii na maarifa ili niweze kufikia ufaulu wa hali ya juu.

**Tarehe ya kuzaliwa** ____________________ **Dini yake** _________________
**Dhehebu** ______________________________
**Sahihi ya Mwanafunzi** __________________ **Tarehe:**____________________

(II) **MZAZI/MLEZI.**

Mimi ______________________________ Mzazi/Mlezi wa ______________________ Nitahakikisha mwanangu anafuata hayo yote yaliyoelekezwa hapo juu na nitamlipia ada na mahitaji binafsi kama ilivyoelekezwa katika barua ya kujiunga na shule. Naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule katika vikao vya wazazi, wito wa masuala ya nidhamu na mahafali. Pia nakubali mwanangu ashiriki katika safari zote za shule kama vile za kimasomo, michezo, dini n.k.

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi** ______________________ **Tarehe** _____________
**Anuani** ____________________________________
**Simu Na** __________________________________
**E -mail- Address** __________________________

(III) Uongozi wa Shule umepokea tamko hili na linathibitishwa na kusainiwa na;-

**Jina la Mpokeaji** ________________________________ **Tarehe** _____________

**Sahihi** __________________ **Mhuri** ______________